

MKATABA WA UPANGISHAJI

MWANZA-BUHONGWA

Mkataba huu umefungwa leo hii tarehe 10 Mwezi 03 mwaka 2025 kati ya Bwana **JANUARY S. LUGANGIKA**, wa S.L.P MWANZA (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "MPANGISHAJI") kwa upande mmoja na ndugu **MAXILIP INVESTMENT LIMITED** wa S.L.P MWANZA (ambaye katika Mkataba huu anajulikana kama "MPANGAJI") kwa upande wa pili.

IMEKUBALIKA KAMA IFUATAVYO

1. **KWAMBA**, Mpangishaji anamiliki Kitalu M Plo No. 44 kilichopo Kata ya Buhongwa mtaa wa Kishila Jiji la MWANZA Wilaya ya Nyamagana .
2. **KWAMBA**, Mpangishaji ambaye ni mtu mzima na mwenye akili timamu anadhamiria kupangisha kiwanja tajwa hapo juu.
3. **KWAMBA**, Mpangaji amehiari kupanga kiwanja tajwa hapo juu kwa ajili ya **UWEKEZAJI**, hivyo basi pande zote mbili kati ya mpangishaji na mpangaji zimekubaliana kama ifuatavyo;
 - a) Kodi ya pango ni Tsh.500,000 kwa mwaka na mpangaji amelipa kiasi Tsh.2,000,000/= kwa muda wa miaka minne (4) TU. Baada ya miaka minne (4) tutakaa kikao kuangalia gharama za upangishaji upya.
 - b) Mpangaji atakae shindwa kulipa kwa wakati zaidi ya mara mbili basi Mpangishaji hatoweza kuendelea na Mkataba mwingine mpya.
 - c) Mpangaji atazingatia mazingira ya eneo tajwa hapo juu, pamoja na usafi ikiwemo kutotupa taka ovyo.

- d) Mpangaji ndiye atakaye shughulikia miundombinu ya umeme, maji, na miundombinu mingine atakayoona inamfaa.
- e) Baada ya mkataba huu kufungwa MAXILIP INVESTMENT LIMITED atambulike kuwa ni mpangaji halali wa eneo tajwa hapo juu.
- f) Mkataba huu umeanza rasmi Tarehe 30 Mwezi 03 mwaka 2025 na utamalizika tarehe 29 Mwezi 03 Mwaka 2029.
- g) Ikiwa itatoke kutoelewana baina ya Mpangishaji na Mpangaji basi kikao cha usuluhishi kitakaa chini ya uongozi wa serikali ya mtaa wa Kishila.

Kwa kudhibitisha makubaliano hayo yote, paunde zote mbili zimeweka sahihi zao kama ifuatavyo;

MKATABA UMESAINIWA na
JANUARY S. LUGANGIKA
Namba ya simu 0767369250


MPANGISHAJI

MKATABA UMESAINIWA na
MAXILIP INVESTMENT LIMITED
Leo tarehe 10 mwezi 03 mwaka 2025
0764881960.


MPANGAJI

MAXILIP INVESTMENT CO. LTD
P.O. BOX 11028
MWANZA

Mbete fangu :-
Bluso Mwanza
Kamishna
10/3/2025

